**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Ofisi ya Bunge

S.L.P 941

**DODOMA**

18 APRILI, 2017

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, yalipitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya uchambuzi wa Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1), kwa kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2015/16. Baada ya kutimiza sharti hilo,

Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa fedha 2016/2017. Taarifa hiyo inahusisha jumla ya Mafungu Ishirini na Nane (28) kama ifuatavyo:-

i. Fungu 56: Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

ii. Fungu 02: Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC); na

iii. Mafungu 26 ya Mikoa yote ya Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya uchambuzi wa Taarifa ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii yaliyowasilishwa, Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais – TAMISEMI inajikita katika maeneo manne yafuatayo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA NA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilitengewa jumla ya **Shilingi 1,630,731,452,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuzingatia sharti la kipindi kisichozidi siku Saba (7) ambalo limewekwa na Kanuni, Kamati ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Baadhi ya miradi hiyo, inahusu Mpango wa Miji Mkakati Tanzania (*Tanzania Strategic Cities Project – TSCP*); Mfuko wa Barabara (*Road Fund*); Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake (Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri) na Ukarabari na Uendelezaji wa Hospitali za Mikoa. Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 Mradi Na. 6403 - Tanzania Strategic Cities Project (TSCP).

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 8,042,405,000** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8071 cha **Fungu 86** – Mkoa wa Tanga, na **Fungu 78** – Mkoa wa Mbeya. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 55 na unalenga kuboresha miundombinu ya barabara kwa kujenga kwa kiwango cha lami ngumu, kuweka taa za barabarani, kujenga vituo vya Mabasi na mifereji ya maji taka katika Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mbeya. Aidha, mradi unaendelea na ujenzi wa Dampo kubwa la kisasa la kukusanyia taka ngumu katika Jiji la Mbeya, na Maabara ya Vifaa vya Ujenzi katika Jiji la Tanga.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, mradi huu unatekelezwa katika Miji Saba nchini ambayo ni Arusha, Mwanza, Mbeya, Tanga, Dodoma, Mtwara Mikindani, na Kigoma (Ujiji) na Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma (CDA). Ili kujiridhisha na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo Sita (6) kwenye Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mbeya.

### 2.1.2 Mradi Na. 4170 – Mfuko wa Barabara (Road Fund).

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 12,395,296,399** na unatekelezwa kupitia Akaunti Maalum ya Mfuko wa Barabara katika Fungu 86: – Mkoa wa Tanga; Fungu 73: – Mkoa wa Iringa na Fungu 79: – Mkoa wa Morogoro.

Mfuko huu ulianzishwa mwaka 1992 kwa lengo la kukarabati, kuboresha na kutengeneza barabara muhimu za Mikoa, Wilaya na Mijini, kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato kama vile tozo na ushuru katika matumizi ya barabara na mafuta, leseni na usajili wa magari. Mfuko huu umekuwa ukisimaiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

**Mheshimiwa Spika, u**tekelezaji wa mradi huu unalenga kuboresha miundombinu ya barabara, matengenezo ya barabara ya kawaida na sehemu korofi kwa kujenga kwa kiwango cha lami, kujenga vituo vya mabasi, mifereji ya maji taka, madaraja na kuwajengea uwezo wataalam wa

barabara waliopo katika sekretarieti za Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ili kujiridhisha na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika mradi huu, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo Sita yaliyoko kwenye Mikoa ya Tanga, Morogoro na Iringa.

### 2.1.3 Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulitengewa jumla ya **shilingi 460, 589, 216, 216** na unatekelezwa chini ya kifungu 8091 cha Fungu 78: - Mkoa wa Mbeya; Fungu 54: Mkoa wa Njombe na Fungu 86: Mkoa wa Tanga. Mradi unalenga kusaidia Vikundi vya Wanawake na Vijana kupitia Halmashauri kwa kutenga asilimia kumi (10%) ya mapato ya Ndani ya Halmashauri, kwa ajili Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake.

Ili kujiridhisha na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika mradi huu, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo matano (5) katika Mikoa ya Tanga, Mbeya na Njombe.

### 2.1.4 Mradi Na.5402 – Ukarabati na Uendelezaji wa Hospitali za Mikoa (Regional Hospital Rehabilitation)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa **shilingi 1,342,700,000** na unatekelezwa chini ya Kifungu cha 3001 cha Fungu 86 – Mkoa wa Tanga, na Fungu 78: - Mkoa wa Mbeya. Kwa mujibu wa Taarifa zilizowasilishwa kwenye

Kamati, Mradi huu umekuwa ukilenga kukarabati na kuendeleza majengo ya Hospitali za Mikoa ili kuziwezesha kutoa huduma ya rufaa katika hospitali hizo.

Ili kujiridhisha kuhusiana na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo mawili (2) katika Mikoa ya Tanga na Mbeya.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha tija ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha unaoisha, ni muhimu kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya ukaguzi huo. Kwa madhumuni hayo taarifa hii imetumia njia kadhaa ikiwa ni pamoja na majedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji ili kubainisha hali ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Ofisi hii. Ufafanuzi wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:

### 2.2.1 Mradi Na. 6403 - Tanzania Strategic Cities Project (TSCP).

**Mheshimiwa Spika,** katika maeneo Sita yaliyoko kwenye Halmashauri za Majiji ya Mbeya na Tanga, ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa Mradi huu wa Miji ya Kimkakati (*Tanzaia Strategic Cities Project*), mambo kadhaa yalibainika kuhusiana na utekelezaji huo, ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kujua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza. Kutokana na ukaguzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

**a) Mafanikio;**

i) Kuongezeka kwa kilomita za barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami. Mfano; katika Jiji la Mbeya barabara hizo zimeongezeka kutoka kilomita 29 zilizokuwepo kabla ya kuanza kwa mradi huu hadi 52.1 (ongezeko hilo ni sawa na asilimia 79.65);

ii) Kuboreshwa kwa mandhari ya Majiji ya Mbeya na Tanga;

iii) Kupanda thamani kwa viwanja na majengo yaliyo jirani na miradi ya TSCP;

iv) Vituo vya Mabasi ambavyo vimejengwa kupitia mradi huu, vimesaidia kuondoa kero ya usafiri kwa kupunguza msongamano wa mabasi;

v) Fursa za biashara, kwa maeneo yaliyo kando na miradi ya TSCP;

vi) Dampo la kukusanyia Taka, limechangia kuweka maeneo ya Jiji la Mbeya katika hali ya usafi;

**b) Changamoto;**

i) Kukosekana kwa mifereji ya kuondoa maji ya mvua kwenye barabara zilizojengwa na mradi

huu, na hivyo kusababisha maji kutuama kwa muda mrefu na hivyo kuharibu barabara;

ii) Baadhi ya madereva wasio waaminifu wamekuwa wakipitisha magari yenye uzito zaidi ya unaotakiwa kwenye barabara zilizojengwa. Mfano; barabara za Kabwe – Block T, Kisanji na Sae – Ituha, za Jijini Mbeya zimejengwa kwa ajili ya magari yasiyozidi Tani 10. Hata hivyo, madereva wa magari wasiozingatia alama za barabarani wamekuwa wakipitisha magari yenye uzito zaidi;

iii) Kupasuka mara kwa mara kwa mabomba yaliyokatisha kwenye barabara, kunasababisha uharibifu kwenye maeneo hayo ya barabara. Mfano ni barabara ya Ilomba – Isyesye na Airport – Samora, katika Jiji la Mbeya; na

iv) Wizi wa karatasi ngumu katika eneo linalosaidia kuhifadhi taka kwenye Dampo la kisasa, katika jiji la Mbeya.

### 2.2.2 Mradi Na. 4170 – Mfuko wa Barabara (Road Fund).

**Mheshimiwa Spika,** katika maeneo Sita (6) ya Mikoa ya Tanga, Morogoro na Iringa, ambayo Kamati iliyatembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu, mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto.

**(a) Mafanikio;**

i. Kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami, na changarawe katika mikoa husika. Mfano; katika Jiji la Tanga, Mfuko wa Barabara umetengeneza kilomita Tisa za barabara kwa kiwango cha changarawe;

ii. Kuwezesha barabara za maeneo korofi kupitika katika muda wote wa mwaka;

iii. Kutengeneza mifereji kwa ajili ya maji ya mvua na hivyo kuepusha uharibifu wa barabara unaosababishwa na maji kutuama;

iv. Wataalam wa barabara katika Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, wamejengewa uwezo;

vii) Kufungua mawasiliano ya barabara kwa kujenga madaraja katika maeneo ambayo mvua zinaharibu barabara na kuvunja madaraja. Mfano; katika mkoa wa Iringa, madaraja 11 yamejengwa katika mwaka wa fedha 2015/16.

(b) **Changamoto;**

i. Kuchelewa kwa fedha za mfuko wa barabara na hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa;

ii. Kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya mfuko wa barabara, kutokana na urasimu wa kuhamisha miundombinu ya maji safi na mati taka, pamoja na nguzo za Umeme;

iii. Upungufu wa Wahandisi wa barabara, katika halmashauri, jambo linalosababisha usimamizi hafifu na kukosekana kwa ushauri wa kitaalam, katika miradi. Mfano; Mkoa wa Iringa una Wahandisi 12 tu kati ya 20 wanaohitajika. Upungufu huo ni sawa na asilimia 60 ya mahitaji.

iv. Uchache wa mitambo ya kutengenezea barabara kwenye halmashauri nyingi nchini, jambo linalosababisha utegemezi wa mitambo ya kukodi na hivyo kuongeza gharama za miradi;

v. Uharibifu wa mara kwa mara wa miundombinu unaosababishwa na mvua na hivyo kuhitaji ukarabati wa mara kwa mara; na

vi. Baadhi ya miradi kutekelezwa chini ya kiwango.

### 2.2.3 Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mradi huu, katika maeneo matano maeneo matano (5) ambayo Kamati iliyatembelea kwenye Mikoa ya Tanga, Mbeya na Njombe, mambo kadhaa yalibainika yakijumuisha mafanikio na changamoto. Ufafanuzi zaidi unatolewa kupitia **Jedwali Na.01**

**Jedwali Na.01:** Mikoa na Vikundi vilivyopata mikopo kutoka Asilimia Kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri.

| Mkoa | Fungu | Vikundi vilivyokopeshwa | Fedha iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| Tanga | 86 | 27 | 66,000,000 |
| Mbeya | 78 | 52 | 101,600,000 |
| Njombe | 54 | 197 | 292,989,216 |
| **Jumla** | | **276** | **460,589,216** |

Chanzo: Taarifa za Mikoa ya Tanga, Mbeya na Njombe.

**(a) Mafanikio;**

i. Wanawake na Vijana wamewezeshwa kupata elimu ya ujasiriamali na mikopo ya kuanzisha miradi ya kiuchumi;

ii. Wanufaika wameweza kuongeza kipato na hivyo kuboresha hali ya maisha;

iii. Baadhi ya vikundi vimeanzisha vyama vya kuweka na kukopa (SACCOs) kupitia fedha hizi, na kukuza mtaji ili kuongeza wigo wa mikopo katika jamii. Mfano ni Kikundi cha Nyombo, katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ambacho kilianzisha SACCOs mwaka 1999 kwa mtaji wa **shilingi milioni 1.4** na hadi mwezi Februari, 2017 mtaji huo ulikuwa umeongezeka hadi kufikia **shilingi bilioni 1.58**; na

iv. Kupungua kwa uhalifu kwani Vijana wanapata mitaji inayowawezesha kuanzisha shughuli za kuwaingizia kipato;

(b) **Changamoto;**

i. Kukosekana kwa sheria inayosimamia utekelezaji wa Agizo la Serikali la kuzitaka Halmashauri kutenga kikamilifu asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Vijana na Wanawake;

ii. Halmashauri kutumia sehemu ya mapato yanayotokana na asilimia kumi (10%) ya Mapato ya ndani, kutekeleza shughuli nyingine, na hivyo kuwanyima Vijana na Wanawake fursa ya kupata mikopo;

iii. Baadhi ya Vikundi vya Wanawake na Vijana kutorejesha fedha kikamilifu ili kutoa fursa kwa wengine kukopeshwa;

iv. Baadhi ya Vijana na Wanawake kukosa elimu ya ujasiriamali na hivyo kushindwa kuendesha miradi wanayoianzisha;

v. Halmashauri kukosa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa kutosha kwa ajili ya kuelimisha Vijana na Wanawake wanaonufaika na mikopo hii; na

vi. Vijana na Wanawake kukosa maeneo rasmi ya kuendeshea shughuli wanazoanzisha kutokana na mikopo wanayopewa na mpango huu.

### 2.2.4 Ukarabati wa Hospitali za Mikoa *"Regional Hospital Rehabilitation"*

**Mheshimiwa Spika,** katika Hospitali mbili za Mikoa ambazo Kamati ilitembea katika Mikoa ya Tanga na Mbeya, ili kukagua utekelezaji wa mradi huu, mambo yafuatayo yalijiri:-

**(a) Mafanikio;**

i. Kujengwa kwa baadhi ya majengo muhimu kama vile jengo la ICU (Hospitali ya Mkoa wa Tanga);

ii. Ukarabati wa majengo chakavu na kuanza kutumika. Mfano; Hospitali ya Mkoa wa Tanga imekarabati jengo la Grade One kwa **shilingi milioni 28** na sasa linatumika;

iii. Hosptali ya Mkoa wa Mbeya imefanikiwa kujenga mita 429 za njia za kupitia wagonjwa (*walk ways*); na

iv. Ununuzi wa gari la kubebea wagonjwa mahututi kwa hospitali ya Mkoa wa Tanga.

**(b) Changamoto;**

i. Bajeti finyu inayotengwa na kutopatikana kikamilifu;

ii. Hospitali kukabiliwa na msongamano mkubwa wa wagonjwa;

iii. Kukosekana kwa huduma muhimu za tiba kwa ukosefu majengo. Mfano; Hospitali ya Mkoa wa Mbeya, haina majengo ya Huduma muhimu za tiba Tisa, miongoni mwa hayo ni jengo la huduma ya dharura (*casualty*) na upasuaji (*theatre*);

iv. Barabara za kikamilifu kwa fedha hizo. Mfano; kati ya **shilingi milioni 467** zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Wodi ya Upasuaji katika hospitali ya Mkoa wa Mbeya, ni **shilingi milioni 200** tu ndiyo ilikuwa imetolewa hadi mwezi Februari, 2017. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 42.82** ya kiasi kilichotengwa.

v. Uchakavu wa majengo;

vi. Ukosefu wa vifaa kama Ct Scan, Echo na vitendanishi vya maabara;

vii. Bajeti finyu kwa ajili ya dawa; na

viii. Ukosefu wa Wodi ya Wagonjwa mahututi.

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, ni maoni ya Kamati kwamba:-

i. Miradi ya maendeleo ingetekelezwa kikamilifu na kukamilika kwa wakati iwapo fedha zilizotengwa zingetoka kwa wakati na kiasi cha kutosha;

ii. Urasimu katika Halmashauri unachelewesha hatua muhimu za utekelezaji wa miradi;

iii. Uelewa wa kutosha juu ya uendeshaji wa miradi pamoja na ushirikishwaji wa Wananchi utasaidia Wananchi kuanzisha miradi na kuifanya kuwa endelevu;

iv. Kukosekana kwa umakini na upembuzi yakinifu wa kutosha kwenye miradi ya maendeleo, kunaisababishia Serikali hasara kutokana na kuongezeka kwa gharama za miradi;

v. Kukosekana kwa ufanisi wa kitaalam katika usimamiaji wa miradi ya maendeleo kunasababisha miradi hiyo kutekeleza chini ya kiwango;

vi. Matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, yamechangia kuongezeka kwa makusanyo ya Serikali na kudhibiti mianya ya upotevu;

vii. Kukosekana kwa maeneo maalum ya kufanyia biashara na shughuli za uzalishaji, kunakwamisha juhudi za kuwakwamua kiuchumi Vijana na Wanawake;

viii. Kukosekana kwa elimu ya usajiriamali kwa Vijana na Wanawake, kunawakwamisha kujikwamua kiuchumi;

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kwa kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati, pamoja na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati vikao vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ufafanuzi wa ziada kuhusu uchambuzi huu, Kamati imetumia majedwali ili kurahisisha maelezo yake wakati wa kuonesha taarifa, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji.

#### 3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais – TAMISEMI ( Fungu 56) ilitarajiwa kukusanya jumla ya Shilingi **16,880,839,976.00** kutoka vyanzo vya ndani. Mapato haya yalitarajiwa kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni

pamoja na vifaa chakavu, na kwa upande wa Taasisi mapato yalitarajiwa kutokana na tozo mbalimbali, ukusanyaji wa madeni, makusanyo ya mapato yatokanayo na nauli za mabasi, ada za Wanafunzi katika Vyuo, ushuru wa mauzo ya bidhaa mbalimbali, kodi ya pango zinazotozwa kwa wapangaji wa majengo mbalimbali ya taasisi, na mapato yatokanayo na uchangiaji wa huduma za Afya katika hospitali.

Hadi kufikia Februari, 2017 jumla ya **Shilingi 4,750,262,451.03** zilikuwa zimekusanywa na Fungu 56. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 28.13** ya mapato yaliyokadiriwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2016/17. Kamati ilitaka kujua ni kwanini kumekuwa na kiwango kidogo cha Makusanyo ya maduhuli, na sababu zilizotolewa ni pamoja na:-

i. Mauzo machache ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu vya ofisi, na

ii. Ukusanyaji mdogo wa mapato kutoka vyanzo vingine tofauti na makadirio ya awali.

**Mheshimiwa Spika**, ingawa mwenendo huu wa ukusanyaji wa maduhuli siyo mzuri, hata hivyo, kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa zaidi ya **asilimia 16** ikilinganishwa na kiwango cha **asilimia 12** kilichokuwa kimekusanywa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/16. Kamati inatarajia kuwa, mwenendo huu wa ukusanyaji mapato utaendelea kuimarika katika mwaka ujao wa fedha, 2017/18.

Aidha, ni vyema Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ikakadiria makusanyo kwa kuzingatia hali halisi ya vyanzo vya mapato vinavyotarajiwa, ili kuepusha kutofikiwa kwa malengo yaliyowekwa, jambo ambalo linatoa taswira ya kutowajibika ipasavyo kwa mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato.

### 3.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, umebaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/17 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba:-

i. Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo kuliko ilivyokusudiwa katika Mpango wa upatikanaji fedha *(cash flow plan*); na

ii. Fedha zinazopaswa kutolewa na Hazina hazipatikani kwa wakati, jambo linaloathiri utekelezaji wa Mpango kazi uliowekwa ili kutekeleza malengo ya bajeti ya Ofisi hii;

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2017 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea **Shilingi 202, 297,842,072/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 57 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii.

Ulinganisho wa Kamati kuhusiana na hali hiyo ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2016/17 na mwaka 2015/16 ulibaini kwamba, kiasi hicho cha fedha ni ongezeko la **asilimia 8** ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2015/16 ambapo ulikuwa ni **asilimia 48** ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa kwa kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kilikuwa **Shilingi 18,629,656,339** ambacho ni sawa na asilimia 64 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi hayo. Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa asilimia 18 ikilinganishwa na fedha iliyokuwa imepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawada katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/16 ambayo ilikuwa ni asilimia 46 ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umebaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2017, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zake, ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 183,668,185,733.00** kutoka Hazina, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 56 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa **asilimia 8** ikilinganishwa na kiasi kilichokuwa kimepokelewa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/16 kwa ajili ya maendeleo ambacho kilikuwa ni **asilimia 48** ya kiasi chote kilichokuwa kimeidhinishwa na Bunge lako tukufu katika mwaka huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, ingawa mwenendo wa upatikanaji fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) katika mwaka wa fedha 2016/17 umeonekana kuwa mzuri **(wastani wa asilimia 60.5**) ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2015/16 ambao ulikuwa na **wastani wa asilimia 47**, bado lengo tarajiwa halikufikiwa kikamilifu.

Kwa matarajio ya kawaida upatikanaji wa fedha hadi kufikia robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti unapaswa kuwa zaidi ya asilimia 70, kwa mgawanyo wa angalau asilimia 25 ya upatikanaji fedha katika kila robo.

Aidha, bado upatikanaji fedha kwa ajili ya maendeleo umeendelea kuwa chini ikilinganishwa na fedha zinazotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Tafsiri ya mwenendo huu ni kwamba, tutaendelea kushuhudia ucheleweshwaji katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na ongezeko la gharama za miradi hiyo kwa kipindi cha mwaka kilichosalia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho wa uwiano wa fedha iliyoidhishwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na fedha iliyopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2017, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Ufafanuzi zaidi wa ulinganisho huu umeoneshwa kupitia **Jedwali Na. 02**

**Jedwali Na.02:** Bajeti iliyoidhinishwa dhidi ya Fedha zilizopatikana hadi Februari, 2017

| Mgawanyo | Bajeti ya Mwaka wa fedha 2016/17 | Fedha zilizotolewa hadi Februari, 2017 | Asilimia ya fedha iliyopokelewa hadi Februari, 2017 |
|---|---|---|---|
| OC | 6,396,357,000 | 4,236,929,183 | 66.24 |
| Mishahara | 22,516,917,000 | 14,392,727,155 | 63.92 |
| Maendeleo | 325,469,218,000 | 183,668,185,733 | 56.43 |
| **Jumla** | **354,382,492,000** | **202,297,842,072** | **100** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI

### 3.1.3 Mapito ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Kamati ilitoa ushauri katika mambo Kumi na Tano (15) kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliweza kuzingatia kikamilifu baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati, na inaendelea kufanya hivyo kwa maoni mengine

yaliyosalia. Baadhi ya maoni na ushauri uliozingatiwa ni kuhusu:-

i. Kuhakikisha Halmashauri na Mikoa inatumia kikamilifu Mifumo ya Kielektroniki katika Ukusanyaji wa Mapato ambayo ni *Local Government Revenue Collection Information System* (LGRCIS) na Got - HOMIS ambao ni mahususi katika mapato yanayotokana na uchangiaji katika Sekta ya Afya. Hadi Februari 2017 jumla ya Halmashauri 175 kati ya 185 ambazo ni sawa na asilimia 95 zinatumia mfumo wa LGRCIS, na zilizosaliana ziko katika hatua mbalimbali za ufungaji wa mfumo. Aidha, Hospitali 19 za Rufaa za Mikoa, Hospitali 43 za Wilaya, Vituo vya Afya 38 na Zahanati moja (1) zimefungiwa Mfumo wa GoT – HOMIS;

ii. Uhakiki wa Watumishi hewa na kuwaondoa katika mfumo wa malipo ya mishahara (*Payroll*) ili kuepusha upotevu wa fedha za umma. Hadi mwishoni wa Februari, 2017 jumla ya Watumishi 13,369 waliondolewa katika orodha ya malipo ya mishahara ya Serikali kutokana na sababu za utoro, kustaafu na vifo. Aidha, kati ya Watumishi hao 4,968 walibainika kuwa Watumishi hewa na wameisababishia Serikali hasara ya Shilingi bilioni 25.36. Juhudi za Ofisi ya Rais – TAMISEMI zimefanikiwa kufuatilia na kurejesha Shilingi bilioni 2.7 (sawa na asilimia 11 ya fedha zote) na juhudi zinaendelea ili kurejesha zilizosalia; na

iii. Kukamilisha mfumo wa ukusanyaji nauli kwa njia ya kielektroniki na kupanga nauli ili Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, Dar es Salaam (DART) uanze kutoa huduma kwa Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam. Mfumo huo ulikamilika na kuanza kutumika katika ukusanyaji wa nauli tangu tarehe 16 Mei, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya maoni ambayo yanaendelea kuzingatiwa ni pamoja na:-

i. Kuhakikisha Halmashauri zinatenga kikamilifu asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi Wanawake na Vijana. Serikali inaendelea na utekelezaji wa agizo hili kwa kuliingiza katika mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 ili kuipa nguvu ya kisheria Mifuko ya Maendeleo ya Vijana na Wanawake. Rasimu ya kwanza ya mapendekezo hayo imefikishwa katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, na inasubiri kuendelea na hatua zinazofuata; na

ii. Kuhakikisha fedha za maendeleo hazichelewi kutoka Hazina. Bado jambo hili halijatekelezwa kikamilifu kwani fedha za maendeleo zinaendelea kuchelewa. Hadi mwezi Februari 2017, ni asilimia 56 tu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ndiyo zilikuwa zimetolewa na Hazina.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inayojumuisha Mafungu 28 (Fungu 56; Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020; Malengo Endelevu ya Maendeleo *(Sustainable Development Goals*); Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI uliofanyiwa mapitio mwaka 2016; Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inapanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha amani na utulivu nchini na kusimamia shughuli za utawala bora na kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D)

ii. Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI ;

iii. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi (Core Business) ya kila Taasisi yaliyoainishwa kwenye Mipango Mikakati yao;

iv. Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji hasa katika kilimo na viwanda ;

v. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikiwa ni pamoja kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ;

vi. Kuratibu shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimu, afya na sekta nyingine;

vii. Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Serikali katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri, pamoja na kuendeleza rasilimali watu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi; na

viii. Kusimamia, kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Taasisi, programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 6, 568, 841, 586,637**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4, 535, 390, 860,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 1, 779, 128, 523,846** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 4,270,265,560,000,** sawa na asilimia 89.15 ni kwa ajili ya mishahara, na **Shilingi 519,447,430,791,** sawa na asilimia

10.85 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. **Jedwali Na. 03** linafafanua zaidi juu ya Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Jedwali Na. 03** Mgawanyo wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

| MGAWANYO | BAJETI MWAKA WA FEDHA 2017/18 | Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya Wizara |
|---|---|---|
| Matumizi Mengineyo | 519,447,430,791 | 7.92 |
| Mishahara | 4,270,265,560,000 | 65.00 |
| Maendeleo | 1,779,128,523,846 | 27.08 |
| **Jumla** | **6,568,841,586,637** | **100** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI

### 4.2 Uchambuzi wa makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, inakadiria kukusanya jumla ya shilingi **713,187,789,615.** Mapato hayo yameongezeka kwa **Shilingi 30,575,512,826** sawa na **asilimia 4.48** ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha

2016/2017 kwa mgawanyo utakaooneshwa katika **Jedwali Na. 04** hapo chini.

**Mheshimiwa Spika,** makusanyo hayo yanatarajiwa kutokana na kuuza vifaa chakavu pamoja na nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, marejesho ya masurufu na mishahara. Aidha, kwa upande wa Halmashauri, makusanyo yatatokana na ushuru na kodi mbalimbali na vyanzo vingine vya mapato vilivyopo kwa mujibu wa sheria.

**Jedwali Na. 04 Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo ya ndani**

| Ofisi/Taasisi | Bajeti 2016/17 | Bajeti 2017/18 | Ongezeko | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| OR-TAMISEMI na Taasisi | 16,867,336,976 | 22,766,063,908 | 5,898,726,932 | 34.97 |
| Mikoa | 330,111,813 | 3,115,064,707 | 2,784,952,894 | 843.63 |
| Halmashauri (MSM) | 665,744,939,813 | 687,306,661,000 | 21,891,833,000 | 3.29 |
| **JUMLA KUU** | **682,612,276,789** | **713,187,789,615** | **30,575,512,826** | **4.48** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa uchambuzi, sehemu kubwa ya makusanyo inatarajiwa kupatikana kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sababu kubwa kuhusiana na kiasi hicho kikubwa cha makusanyo ni kwamba, Mfumo wa Serikali za Mitaa, ndiyo wenye watu wengi na unamiliki vyanzo vingi vya mapato. Aidha, kuanza kutumika kwa mfumo wa ukusanyaji wa Mapato kwa njia ya Kieletroniki kumeonekana kusaidia ongezeko la makusanyo.

Aidha, Mikoa licha ya kuwa na ongezeko kubwa la Makusanyo (asilimia 843.63) bado imeendelea kuwa na makusanyo madogo ikilinganishwa na Halmashauri, na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake.

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinaombewa kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 6,568,841,568,673** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tawala za Mikoa na katika Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo zinazoombwa, **Shilingi 4,789,713,062,791** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,779,128,523,846** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, katika fedha, hizo zipo **Shilingi 12, 422,291,495** kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

**Mheshimiwa Spika**, kiasi cha Fedha kinachoombwa kimeongezeka kwa **Shilingi 516,240,633,637,** sawa na asilimia 8.52% ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na MSM katika mwaka wa fedha 2016/2017. Hata hivyo, ongezeko la mwaka huu ni dogo ikilinganishwa na lililopita, katika mwaka wa fedha 2016/17 ambalo lilikuwa asilimia 12.

Uchambuzi umebaini kwamba, katika fedha za miradi ya maendeleo, kuna ongezeko la **Shilingi 148,397,071, 846** kutoka **Shilingi 1,630,731,452,000** za mwaka wa fedha 2015/2016 hadi **Shilingi 1,779,128,523,846** katika mwaka wa

fedha 2017/2018. Ongezeko hili ambalo ni sawa na **asilimi 9.10** ni dogo sana kwani limepungua kwa zaidi ya mara Saba, ikilinganishwa na ongezeko lililoshuhudiwa katika mwaka wa fedha 2016/17 ambalo lilikuwa ni **asilimia 74. 83**

**Mheshimiwa Spika,** ni jambo lisilopingika kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ndiyo inayoongoza kwa kuwa na bajeti kubwa dhidi ya Wizara nyingine, zikilinganishwa na bajeti ya Taifa. Kwa mfano; katika mwaka wa fedha 2017/2018 bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefikia asilimia 20.72 ya Bajeti ya Taifa ambayo ni takribani **Shilingi Trilioni 31. 699.** Hilo ni ongezeko la **asilimia 0.23** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/17 ambapo ongezeko lilikuwa **asilimia 20. 49.** Hata hivyo, kiwango hicho kinaendelea kuwa pungufu ikilinganishwa na uwiano wa namna hiyo katika mwaka wa bajeti 2015/16 ambapo bajeti ya TAMISEMI ilikuwa ni asilimia 24 ya bajeti yote.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kama unavyooneshwa katika **Jedwali Na. 05**:-

**Jedwali Na 5: Mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya OR- TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 ikilinganishwa na Mwaka 2016/17**

| AINA YA MATUMIZI | 2016/17 | 2017/18 | Ongezeko | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya kawaida** | | | | |
| **OR – TAMISEMI** | | | | |
| Mishahara Makao Makuu | 8,130,978,000 | 8,491,975,000 | 360,997,000 | 4.43 |
| Mishahara ya Taasisi | 14,385,939,000 | 15,318,027,000 | 932,088,000 | 6.47 |
| Matumizi Mengineyo Makao Makuu | 3,835,054,000 | 6,384,732,000 | 2,549,678,000 | 66.48 |
| Matumizi Mengineyo Taasisi | 2,561,303,000 | 1,827,564,296 | -733,738,704 | -28.64 |
| **JUMLA** | **28,913,274,000** | **32,022,296,296** | **3,109,022,296** | **10.75** |
| **Tume ya Utumishi wa Walimu** | | | | |
| Mishahara | 6,442,019,000 | 7,800,146,000 | 1,358,127,000 | 21.08 |
| Matumizi Mengineyo | 3,605,773,000 | 4,622,145,495 | 1,016,372,495 | 28.19 |
| **Jumla** | **10,047,792,000** | **12,422,291,495** | **2,374,499,495** | **23** |

| AINA YA MATUMIZI | 2016/17 | 2017/18 | Ongezeko | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa** | | | | |
| **Mikoa: (Mafungu 26)** | | | | |
| Mishahara | 153,036,181,000 | 168,579,832,000 | 15,543,651,000 | 10.16 |
| Matumizi Mengineyo | 37,786,227,000 | 41,297,783,000 | 3,511,556,000 | 9.29 |
| **Jumla** | **190,822,408,000** | **209,877,615,000** | **19,055,207,000** | **9.98** |
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | | | | |
| Mishahara | 3,593,880,663,000 | 4,070,075,580,000 | 476,194,917,000 | 13.25 |
| Matumizi Mengineyo | 598,205,364,000 | 465,315,280,000 | -132,890,084,000 | -22.21 |
| **JUMLA** | **4,192,086,027,000** | **4,535,390,860,000** | **343,304,833,000** | **8.18** |
| **Mpango wa Maendeleo** | | | | |
| OR-TAMISEMI | 325,469,218,000 | 413,178,629,846 | 87,709,411,846 | 26.95 |
| Mikoa | 64,701,480,000 | 75,259,322,000 | 10,557,842,000 | 16.32 |
| Halmashauri | 1,240,560,754,000 | 1,290,690,572,000 | 50,129,818,000 | 4.04 |
| **JUMLA** | **1,630,731,452,000** | **1,779,128,523,846** | **148,397,071,846** | **9.10** |

| AINA YA MATUMIZI | 2016/17 | 2017/18 | Ongezeko | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA KUU** | **6,052,600,953,000** | **6,568,841,586,637** | **516,240,633,637** | **8.52** |

**Chanzo: Randama ya TAMISEMI**

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

i. Serikali isimamie na kuhakikisha Halmashauri zinaandaa na kutunza takwimu sahihi kuhusiana na Vikundi vya Wanawake na Vijana, na jinsi vinavyopokea na kurejesha fedha zinazotokana na Asilimia Kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri. Aidha, Halmashauri zitekeleze kwa ukamilifu utengaji wa fedha hizo na kuzipeleka kwa wahusika kwani ni Agizo la Serikali na siyo hiyari;

ii. Serikali iangalie uwezekano wa kurejesha sehemu ya mapato yatokanayo na Kodi ya Majengo (*property tax*) katika Halmashauri za Manispaa Thelathini (30) nchini ambazo zimeathirika kutokana na chanzo hicho cha mapato kuchukuliwa na Mamlaka ya Mapato (TRA);

iii. Serikali iruhusu Halmashauri kukata asilimia 30 ya mapato yatokanayo na Kodi ya Ardhi na Asilimia 25 ya Mapato yatokanayo

na Kodi katika Huduma za Misitu, kabla ya kuwasilisha fedha hizo Serikali Kuu, kwani uzoefu unaonesha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuwa hairejeshi fedha hizo kwenye Halmashauri;

iv. Halmashauri zibuni vyanzo vipya vya mapato ili kuepuka kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu. Aidha, vyanzo hivyo vipya vitaziba pengo la mapato yaliyokuwa yakitokana na ushuru mdogo mdogo ulioondolewa na Serikali kutokana na kuwa kero kwa wananchi;

v. Mikoa iandae vipaumbele vichache kulingana na uwezo wa bajeti na kusimamia kikamilifu utekelezaji wake, badala ya kuwa na msururu wa vipaumbele ambavyo havitekelezeki kutokana na ufinyu wa Bajeti;

vi. Halmashauri ziwatumie Maafisa wa Maendeleo ya Jamii kutoa elimu ya ujasiriamali kwa Vijana na Wanawake, ili kuwajengea uwezo wa kuendesha kwa ufanisi miradi ya maendeleo inayoanzishwa na vikundi hivyo na hatimaye kuepusha upotevu wa mitaji wanayopatiwa;

vii. Halmashauri zishirikiane na Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ili kuandaa mpango wa matumizi bora ya Ardhi, kwa kuanisha maeneo ya kilimo, ufugaji na matumizi mengine, jambo litakalosaidia kuepusha migogoro ya ardhi baina ya Wakulima na Wafugaji;

viii. Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati ili kuziwezesha Halmashauri kulipa madeni ya Wazabuni na Wakandarasi kwa wakati na hivyo kuepusha ongezeko la madeni katika miradi inayotekelezwa;

ix. Serikali iandae utaratibu utakaowezesha Halmashauri kukusanya kikamilifu mapato yatokanayo na huduma za minara ya simu pamoja na mabango ya biashara;

x. Serikali iongeze kasi ya kuajiri Wataalam wa Afya na upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Serikali, ili kuwezesha Wananchi kupata huduma stahiki za afya;

xi. Serikali ihakikishe Halmashauri ambazo hazijaanza kutumia mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki, zinafanya hivyo haraka iwezekanvyo ili kuepusha upotevu wa mapato unaotokana na ukusanyaji wa kutumia vitabu. Aidha, halmashauri ambazo hazitumii mfumo huo kikamilifu kutokana na kutokuwa na mashine za kutosha, zihimizwe kununua mashine za kutosha na kuzitumia katika ukusanyaji wa mapato; na

xii. Serikali ipeleke kikamilifu fedha za ukarabati na uendelezaji wa hospitali za Mikoa ili kuziwezesha kukamilisha matengenezo yaliyokusudiwa na kuanza kutoa huduma za afya kikamilifu kwa lengo la kupunguza msongamano wa wagonjwa uliopo.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi za dhati kwako binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkiendesha shughuli za Bunge vizuri. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Mwanne Ismail Mchemba, kwa kuchaguliwa na Wajumbe wa Kamati, kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Hii inaonesha imani kubwa waliyonayo kwake, pamoja na kutambua mchango wake kwa Kamati katika kipindi chote alichokuwa akinisaidia majukumu ya Kamati kabla ya kuchaguliwa rasmi. Ninamshukuru sana kwa ushirikiano wake, na nina imani tutaendelea kushirikiana katika kuitumikia vyema Kamati.

Vilevile, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa weledi na ushirikiano mkubwa waliouonesha wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati, ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa kina wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, 2017/2018.

Kamati hii ina Mafungu mengi ya Bajeti ambayo inayashughulikia, na kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umetengwa wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi ikiwa ni pamoja na siku za mwisho wa wiki. Mazingira hayo magumu hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, na badala yake walijitoa kikamilifu na kukabili majukumu yaliyokuwa mbele yao, kwa moyo na weledi wa hali ya juu wakiashiria utayari wao katika kulitumikia Bunge na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu mkubwa, napenda niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti

2. Mhe.Mwanne Ismail Mchemba,Mb –Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb
6. Mhe.Esther Alexander Mahawe,Mb
7. Mhe.George Malima Lubeleje,Mb
8. Mhe.Halima Ali Mohamed,Mb
9. Mhe.Hamad Salim Maalim,Mb
10. Mhe.Waitara Mwita Mwikwabe,Mb
11. Mhe.Innocent Sebba Bilakwate,Mb
12. Mhe.Josephine Tabitha Chagula,Mb
13. Mhe.Khamis Ali Vuai,Mb
14. Mhe.Maida Hamad Abdallah,Mb
15. Mhe.Hamoud Abuu Jumaa,Mb
16. Mhe.Khalifa Mohamed Issa,Mb
17. Mhe.Hussein Ibrahim Makungu,Mb
18. Mhe.Mariam Ditopile Mzuzuri,Mb
19. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
20. Mhe.Ruth Hiyobi Mollel,Mb
21. Mhe.Saada Mkuya Salum,Mb
22. Mhe.Salum Khamis Salum,Mb
23. Mhe.Venance Methusela Mwamoto,Mb
24. Mhe.Zacharia Paulo Isaay,Mb
25. Mhe.Saed Ahmed Kubenea,Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ningependa kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi

ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Seleman Said Jafo (Mb), pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, hiyo wakiongozwa na Eng. Musa Iyombe, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Aidha, nawashukuru Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini, kwa usimamizi na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha unaoisha, na kwa kuwasilisha vyema mbele ya Kamati, Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Vilevile, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Jumla, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Victor Leonard na Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Mariam Ally, kwa uratibu wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S.Rweikiza (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA**

**NA SERIKALI ZA MITAA**

18 Aprili, 2017